

Vipimo vya Haraka vya Antijeni vya COVID-19: Jinsi ya Kuchukua Sampuli


Ili kuchukua sampuli ya kipimo cha haraka cha antijeni (RATs), watumiaji wanapaswa kufuata maelekezo yaliyaondikwa kwenye kikaratasi cha kifaa. Sambamba na njia ya kuchukua sampuli iliyohibitishwa na Health Canada (kama ilivyo kwenye kikaratasi cha kifaa), watumiaji wanaweza kuchukua sampuli mchanganyiko ya kinywa na pua kwani inaweza kuongeza kiwango cha kipimo.

Yafuatayo yanaangazia hatua za jumla za kuchukua sampuli kwa kutumia ama njia mchanganyiko ya kinywa na pua au njia ya pua.


Sampuli ya kinywa na pua (njia mchanganyiko ya kinywa na pua)

1. Usile, usinywe, usitafune chingamu, usivute sigara kwa angalau dakika 30 kabla ya kuchukua sampuli.
2. Kama una tishu, penga kamasi kabla ya kipimo.
3. Nawa mikono yako na shikilia upande wa pamba tofauti na ncha laini.
4. Ingiza ncha laini ya pamba kati ya mashavu ya ndani na ufizi wa chini na zungusha pamba hiyo mara kadhaa.
5. Kisha, sugua ncha laini hiyo ya pamba kwenye ulimi wako karibia kabisa na koo lako kadri iwezekanavyo.
 - Hiari: Badala ya kusugua mashavu yako ya ndani na ulimi, unaweza kusugua sehemu ya nyuma ya koo na mafindo. Unaweza kutumia kioo kikusaidie kuona mahali unaposugua pamba yako.
6. Inamisha kichwa chako kwa nyuma na ingiza kabisa ncha laini ya pamba moja kwa moja nyuma (sio juu) ya pua yako hadi ifike mwisho (hadi cm 2.5). Hakikisha ncha hiyo laini ya pamba imeingia kabisa ndani ya pua.
7. Zungusha pamba mara kadhaa kwenye kuta za pua na iache humo kwa sekunde chache ili ifyonze majimaji ya puani.
8. Toa pamba hiyo puani mwako na kwa kutumia pamba hiyo hiyo, rudia kwenye tundu lingine la pua.
9. Mara moja weka pamba katika bomba maalum kulingana na maelekezo ya kifaa.

Hatua ya 4 - 5



Hatua ya 6



Sampuli ya pua (njia ya pua)

1. Kama una tishu, penga kamasi kabla ya kipimo.
2. Nawa mikono yako na shikilia upande wa pamba tofauti na ncha laini.
3. Inamisha kichwa chako kwa nyuma na ingiza kabisa ncha laini ya pamba moja kwa moja nyuma (sio juu) ya pua yako hadi ifike mwisho (hadi cm 2.5). Hakikisha ncha hiyo laini ya pamba imeingia kabisa ndani ya pua.
4. Zungusha pamba mara kadhaa kwenye kuta za pua na iache humo kwa sekunde chache ili ifyonze majimaji ya puani.
5. Toa pamba hiyo kwenye pua yako na kwa kutumia pamba hiyo hiyo, rudia kwenye tundu lingine la pua.
6. Mara moja weka pamba katika bomba maalum kulingana na maelekezo ya kifaa.

